**MKATABA WA KUPANGISHA GODOWN**

**(LEASE AGREEMENT)**
**LILILOPO KATIKA KIWANJA NO.79, KITALU 'P' MBULU MISSION KAHAMA MJINI**

Mkataba huu umefanyika leo tarehe **01** Mwezi wa **02** Mwaka **2022**

**KATI YA**

**NALIMI NKADI NALIMI** wa **S.L.P KAHAMA** (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "**MWENYE GODOWN")** kwa upande mmoja;-

**NA**

**WISCAP COMPANY LIMITED** wa **S.L.P KAHAMA** (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **"MPANGAJI")** kwa upande wa pili.

**KWA KUWA;**
**"MWENYE GODOWN"** ni Mmiliki halali wa **GODOWN** lililopo kwenye **KIWANJA NO.79 KITALU "P" MBULU MISSION –KAHAMA MANISPAA** na anayo nia ya kupangisha GODOWN.MPANGAJI ameridhia kupanga kwenye GODOWN tajwa hapo juu.

**MWENYE GODOWN NA MPANGAJI KWAPAMOJA WANASHUHUDIA YAFUATAYO:-**

1. **KWAMBA,**
   a) **GODOWN** limepangishwa kwa kipindi cha miezi thelathini na sita (miaka mitatu) tu kuanzia tarehe **01/02/2022** hadi tarehe **01/02/2025 kwa** gharama ya Milioni Mbili na Laki Nne**(Tshs.2,400,000/=)** kwa mwezi na si vinginevyo.

   b) **KODI YA PANGO** ya mwaka mmoja katika **GODOWN** imelipwa **Tshs.2,400,000/=** kimelipwa kwa **MWENYE GODOWN** kodi ya mwaka mmoja**. MPANGAJI** atakuwa analipa kodi ya mwaka mmoja mmoja**.**

   c) **MPANGAJI** amempatia **MWENYE GODOWN kiasi** cha fedha tajwa hapo juu na **MWENYE GODOWN** anakiri kupokea kiasi cha **Tshs.2,400,000/=** kodi ya mwaka.

2. **MAKUBALIANO MWENGINE NI KWAMBA.**
   i. **MPANGAJI** atatumia **GODOWN** hilo kwa ajili ya kuhifadhi mali zake ,hivyo hataweka kwenye godown hilo vitu vyovyote vya aina ya milipuko ambapo kuwepo kwake kunaweza kuhatarisha usalama wa watu na mali kwa namna moja au nyingine tu.

ELISHA AMOS ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P. O. BOX ... KAHAMA

01/02/2022

ii) **MPANGAJI**ataheshimu sheria zote na taratibu halali zinazokubalika na jamii ili kudumisha usalama wa watu na mali zao.

iii) **MPANGAJI**ataweka GODOWN hilo katika hali ya usafi wa kuridhisha nje na ndani; ikiwa ni pamoja na utunzaji wa kuta, milango, madirisha, nyaya na vifaa vya umeme ambavyo ni **MALI YA TANESCO** vilivyomo kwenye GODOWN,**ANGALIZO;** IWAPO MPANGAJI atasababisha uharibifu wa aina yoyote ndani ya GODOWN atalipa gharama za matengenezo hayo na si vinginevyo.

iv) **MPANGAJI** hawaruhusiwi kumpangisha au kubadilishana upangaji na mtu mwingine (kupasiana pango au Ku-sub-let) GODOWN aliyopangishwa, pia wasije akafanya matengenezo yoyote ya kiujenzi katika GODOWN hiyo bila ya kushauriana na kupata kibali kutoka kwa **MWENYE GODOWN .**

v) **MPANGAJI** atamruhusu **MWENYE GODOWN**au/na **MAOFISA WAKAGUZI WA LUKU** kutoka **TANESCO** kuingia muda na wakati unaofaa (official hours) kuona na kufanya matengenezo yatakayohitajika baada ya kuwasiliana na **MPANGAJI** au **MWAKILISHIWAKE** ili mradi matengenezo hayo hayatachukua muda mrefu au kusababisha uhamishaji wa vifaa ndani ya GODOWN .

3. **PANDE ZOTE ZIMEKUBALIANA KWAMBA**:

(a) **MWENYE GODOWN**atalipa Kodi ya kiwanja (**Land Fee**), Kodi ya Majengo (**Property Tax**) kwa mujibu wa Sheria za Halmashauri ya Mji.

(b) Ifahamike wazi kuwa hakutakuwa na bugudha yoyote kwa **MPANGAJI**kwa kuwa amelipa kodi kama waliyokubaliana katika **MKATABA** huu, HIVYO MPANGAJI atatakiwa kuhakikisha haachi kulipaankara zake kama inavyopaswa UMEME/LUKU & MAJI/KUWASA] na malipo mengine yenye uhusiano na mambo hayo katika shughuli zake.

4. **VILE VILE IMEKUBALIWA NA KUTAMKWA KWAMBA:**

(i) **KWAMBA** Mwenye GODOWNhataweza kuchukua Pangokabla ya muda wa pango kwisha na **MPANGAJI** akitaka kuachia GODOWN hilo kabla ya muda hatakuwa na madai yoyote kwenye fedha ya pango iliyokwisha tolewa iwe imetumika ama vinginevyo.

(ii) Mpangaji atahakikisha kuwa haachi malimbikizo ya tozo ama Ankara zozote endapo watahitaji kutoendelea na Mkataba.

(iii) **MKATABA** huu utaishia tarehe **01/02/2023.**Endapo **MPANGAJI** atapenda kuendelea kupanga GODOWN hilo, itabidi kufanya makubaliano mapya na **MWENYE GODOWN**na watafanya hivyo kwa kutoa taarifa hiyo siku 30 kabla ya mkataba kuisha na hivyo hivyo iwapo **MWENYE GODOWN**ataamua kutokuendelea na **MPANGAJI** tajwa hapo juu atampatia notisi ya siku 30 kabla ya mkataba kuisha na si vinginevyo.

ELISHA AMOS ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P. O. Box 248 KAHAMA

01/02/2022

**PANDE ZOTE ZINASHUHUDIA** kwa kuweka Saini zao hapa kwa tarehe na Mwaka kama ilivyo onyeshwa.

Mkatabahuu umesainiwa na kutolewa na
**NALIMI NKANDI NALIMI**
ambaye namfahamu/ametambulishwa kwangu
..........................................ambaye namfahamu
Leo tarehe 01..Mwezi...02....2022

........................
**MWENYE GODOWN**

**SHAHIDI**
JINA: LUCAS MAZIKU ........................................................ ..................
ANUANI 0766380101 ........................................................ SAINI

Mkatabahuu umesainiwa na kutolewa na
**WISCAP COMPANY LIMITED**
ambaye namfahamu/ametambulishwa kwangu
..........................................ambaye namfahamu
Leo tarehe 01..Mwezi...02....2022

........................
**MPANGAJI**

**SHAHIDI**
JINA: JOSEPH KABIICA ........................................................ ..................
ANUANI KAHOMA ........................................................ SAINI
CHEO: JAMKA ........................................................

**MBELE YANGU**

**JINA** ELISHA AMOS ........................................................

**SAINI** ........................................................

**CHEO** WAKILI ........................................................

**TAREHE** 01.02.2022 ........................................................

ELISHA AMOS
ADVOCATE
NOTARY PUBLIC
&
COMMISSIONER
FOR OATHS
P. O. BOX 248, KAHAMA

**KAMISHINA WA VIAPO/WAKILI**